

Mwongozo mfupi wa skrini wa matiti

Skrini ya matiti ni nini?

Skrini ya matiti (mammogram) hutumia X-rays kuangalia saratani ndogo sana kwenye matiti ambayo haiwezi kuonekana au kuhisiwa na mwanamke au daktari wake. Saratani za matiti ambazo hupatikana wakati ni ndogo sana hutibiwa kwa urahisi zaidi.

Skrini ya matiti pamoja nasi

ni bure

inachukua chini ya dakika 30 kupimwa

ina patikana pote Queensland

hauhitaji rufaa ya daktari

Ili kutazama video kuhusu kile kinachotokea kwenye skrini ya matiti, changanua msimbo wa QR hapa chini. Unaweza kwenda pia kwenye breastscreen.qld.gov.au na tafuta kwenye ukurasa wa 'Kufanya skrini ya matiti'.

Je, nani anaweza kupata skrini ya matiti?

Tunatoa uchunguzi wa matiti kwa wanawake* ambao wako miaka 40 na kuzidi, na hawajaona mabadiliko yoyote kwenye matiti yao.

*na watu wa jinsia tofauti wanaokidhi vigezo vya kustahiki, kama ilivyofafanuliwa kwenye breastscreen.qld.gov.au/should-i-screen/who-can-have-a-breast-screen



Nichanganue



Kuwa na ufahamu wa matiti

Kama kipimo chochote cha uchunguzi, uchunguzi wa matiti hauwezi kupata kila saratani ya matiti. Ni muhimu ujifunze jinsi matiti yako yanavyoonekana na kuhisi, na umwone daktari wako ikiwa utagundua mabadiliko yoyote.

Je, una miaka 50 mpaka 74?

Skrini ya matiti unafaa zaidi kwa wanawake wa umri huu. Wanawake wengi wenye miaka 50 mpaka 74 wanatakiwa kupata skrini ya matiti kila miaka 2.

Je, una miaka 40 mpaka 49 au 75 na zaidi?

Kuna hatari na faida tofauti za skrini matiti kwa wanawake katika umri huu. Ongea na daktari wako ili kujua ikiwa skrini wa matiti ni sawa kwako.

Je, uko chini ya miaka 40?

Hatutoi uchunguzi wa matiti kwa wanawake walio chini 40. Uchunguzi wa matiti haufanyi kazi kwa wanawake walio chini ya miaka 40 na hatari ya saratani ya matiti ni ndogo sana.

Matokeo

Wanawake wengi wanatumia matokeo yao 2 ndani ya wiki kadhaa ya skrini za matiti. Pia tutatuma matokeo yako kwa daktari wako ikiwa umetupa maelezo yake. Ikiwa unahitaji vipimo vya ufuatiliaji, mmoja ya wauguzi wetu atakupigia kuzungumza juu ya kile kinachofuata.

Ni watu 6 katika kila wanawake 1000 ambao wana skrini ya matiti watapatikana na saratani ya matiti.

Kufanya miadi au kwa maelezo zaidi nenda kwa breastscreen.qld.gov.au or call 13 20 50



Piga 13 14 50 kupata mkalimani



Queensland
Government